FAINI KWA MWANANCHI ALIYEJENGA BILA KIBALI

Mwananchi atakaejenga bila kibali atatozwa faini ya asimilia mbili (2%) ya thamani ya maendelezo yaliyofanyika katika kiwanja kwa mujibu wa tathmini itakayoandaliwa na mthamini wa Halmashauri. Sheria ndogo za Halmashauri za mwaka 2021 na Sheria ya Mipangomiji Na 8 ya mwaka 2007 kifungu cha 34(1),(2) na (3) vinaelekeza kupigwa faini kwa mwendelezaji yeyote anayekiuka masharti ya uendelezaji Ardhi.

Aidha, kifungu hiki kinatiwa nguvu na sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 kifungu cha 3 – Kanuni za Adhabu (Tangazo la Serikali Na. 84 la mwaka 2001) \

8. ADA YA MABANGO

Ada ya mabango hii hutozwa wafanyabiashara wanaotangaza biashara zao kwa njia ya mabango.

Mabango yote kuanzia futi 1 yanapaswa kulipiwa ushuru Halmashauri,Mhandisi atafanya vipimo na baadae mhasibu atafanya mahesabu kulingana na vipimo vya bango kutoka kwa mhandisi na kupata gharama halisi ambayo mteja atapaswa kulipa. Kwa mabanngo makubwa ya barabarani (billboards) wateja wanapaswa kupata kibali kutoka kwa wakala wa barabara Tanzania na baadae kulipia Halmashauri.

VIWANGO VYA ADA KULINGANA NA AINA YA MABANGO

S/N	AINA YA BANGO	GHARAMA KWA SQ METER (FUTI)
1	Bango ambalo haliwaki	7,000
2	Bango linalowaka	10,000
3	Bango/tangazo la ukutani (Kama vile stika	10,000
4	Matangazo ya TV za barabarani	10,000
5	Stika zinazotangaza bidhaa zilizobandikwa kwenye magari	10,000
6	Ada ya maombi ya kutangaza	4,000
7	Bango la matangazo ya biashara yanayowekwa nje ya eneo la biashara	7,000 (lisilowaka) 10,000 (linalowaka)
8	Vipeperushi vya kutangaza biashara kuanzia idadi ya 100	50,000
9	Tangazo la bango (Promotion)	50,000

9. SHUGHULI ZA BURUDANI NA MICHEZO

"Kibali cha Burudani ni ruhusa ya maandishi yenye masharti inayotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kuendesha sherehe, shughuli, michezo yoyote inayokutanisha watu zaidi ya wawili katika kumbi,uwanja wa michezo, barabarani au sehemu yoyote ya wazi ambapo sauti ya juu itajitokeza.

Kila mtu au taasisi yeyote isiyokuwa ya kiserikali au kidini itakayoendesha shughuli za burudani, italazimika kuomba kibali na kulipia kibali cha kuendesha shughuli hiyo kutoka Halmashauri

Kibali hicho kitaonesha-

(a) sehemu itakayofanyika shughuli hiyo;
(b) muda wa kuanza na kumalizika kwa shughuli hiyo;
(c) aina ya Shughuli au burudani.

NB: Nakala ya kibali hicho itapelekwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya (OCD) ikiwa na viambatisho vyote husika.

ADHABU / FAINI

Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilling laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shillingi millioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja.

ADA NA USHURU UTOKANAO NA SHUGHULI ZA BURUDANI NA MICHEZO

NA.	TUKIO LA BURUDANI	ADA/USHURU (Tsh)	MUDA
1	Kibali cha Tamasha lisilo na kiingilio	100,000.00	Ada zote kwa siku
	lenye kiingilio	200,000.00	
	lenye kiingilio na matangazo	400,000.00	
2	Usajili wa Vikundi vya Sanaa, kwaya na kaswida	85,000.00	Kwa usajili
3	Kibali cha uandaaji Kongamano	80,000.00	Ada zote kwa siku
4	Usajili wa vibanda vya Filamu	100,000.00	Kwa mwaka
5	kibali cha kuchezesha michezo ya kubahatisha kwa kutumia mashine	20,000.00	kwa kila mashine kwa mwaka
6	kibali cha mchezo wa Pool table	30,000.00	kwa kila meza kwa mwaka
7	Kibali cha Tamasha la maonesho (biashara)	50,000.00	Ada zote kwa siku
8	Bahati nasibu ndogo ndogo (fete)	50,000.00	Kwa siku katika eneo moja
9	Mshereheshaji	50,000.00	Kwa tukio
10	Mpambaji wa Ukumbi wa Burudani (harusi, sherehe za jikoni,sherehe za kuaga binti na nyinginezo)	50,000.00	Kwa tukio
11	Mtoa Burudani (DJ)	50,000.00	Kwa tukio
12	Mmiliki wa Kumbi mbalimbali	50,000.00	Kwa tukio moja kwa siku
13	Mpishi wa vyakula	50,000.00	Kwa tukio moja kwa siku
14	Picha Jongefu na Mnato	50,000.00	Kwa tukio moja kwa siku
15	Mnada wa hadhara	50,000.00	Kwa tukio moja kwa siku
16	Harusi na sherehe za kijamii	50,000.00	Kwa tukio moja kwa siku
17	Ada ya Matangazo		Ada zote kwa siku
	(a) Kibiashara na matangazo	200,000.00	
	(b) Yasiyo na biashara	100,000.00	
18	Kukodi Uwanja wa Mpira Furahisha		kwa siku moja tu
	(a)kwa matukio yasio ya kibiashara au hayana ufadhili	100,000.00	
	(b) kwa matukio ya Kibiashara au yenye ufadhili	200,000.00	
19	Play Station	20,000.00	kwa mwezi

10. HUDUMA YA USAFISHAJI WA MAZINGIRA NA UZOAJI TAKA

Ni jukumu la Mkurugenzi kutoa huduma ya usafishaji wa mazingira pamoja na uzoaji taka kwa mujibu wa sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009. Aidha sheria hii inampa mamlaka Mkurugenzi kutoa huduma hii moja kwa moja au kuwapatia wazabuni watoe huduma katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela.

TOZO ZA HUDUMA YA UZOAJI TAKA

Ada za uzoaji taka zinatozwa kwa mujibu wa sheria ndogo za usafi wa mazingira za Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2022.

S/N	AINA YA BIASHARA	ADA YA MWEZI
1	Kaya	3000
2	Biashara mbalimbali	300 - 200,000
3	Taasisi	10,000 - 40,000
4	Viwanda	10,000 – 40,000 kwa tani ya taka

UKIUKWAJI WA SHERIA NDOGO YA USAFISHAJI WA MAZINGIRA.

Kwa kuwa sheria hii inamtaka mwanachi atimize wajibu wake kama ilivyofafanuliwa hapo juu, Endapo mwananchi ataenda kinyume, yafuatayo yatamkabili:

- Atandikiwa hati ya madai au kusudio la mashita ili atimize wajibu wake ndani ya siku saba.
- Akishindwa atashitakiwa kwa mujibu wa sheria ndogo.
- Ikidhibitika pasipo shaka na kutiwa hatiani, atawajibishwa kwa mujibu wa sheria ndogo ya usafi wa mazingira.

ADA YA UKAGUZI WA AFYA

S/N	AINA YA BIASHARA	ADA YA MWEZI
1	Baa, maduka ya vinywaji	
	(groceries) na migahawa	50,000/-
2	Mama lishe	10,000/-
3	Nyumba za wageni (Guest house)	50,000/-
4	Kumbi za starehe au mikutano	10,000/-
5	Hoteli	100,000/-
6	Kiwanda	100,000/-
7	Majengo mengine ya biashara	10,000/-
8	Viwanda vya matofali	50,000/-
9	Ukaguzi wa matofali	20,000/-

LIPA KODI KWA WAKATI , EPUKA FAINI KODI YAKO MAENDELEO YAKO

Imetolewa na Ofisi ya Mkurugenzi
Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela
S.L.P 735, ILEMELA
MWANZA

: Ilemelamc www.ilemelamc.go.tz

#Imetolewa na Ofisi ya Mkurugenzi

Tozo Mbalimbali za halmashauri

YA MANISPAA YA ILEMELA

FAHAMU KUHUSU TOZO MBALIMBALI ZA HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

1. LESENI YA BIASHARA

Je, Leseni ni nini? Leseni ya Biashara ni Kibali anachopaswa kuwa nacho mfanyabiashara kinachodhihirisha kuwa kakidhi vigezo vyote vinavyomruhusu kujihusisha na kuendesha biashara.

Leseni hii hutolewa kwa biashara zote halali mfano migahawa, maduka, bucha n.k na leseni hii hudumu kwa muda wa mwaka mmoja kuanzia tarehe iliyolipiwa

ADA ZA LESENI ZA BIASHARA

Jedwali la aina za Biashara na ada zinapatikana katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2014 **(Pakua/Download: Finance Act 2014).**

Adhabu za kutokuwa na leseni/kuchelewa kulipia leseni.
Adhabu / Penalty yakuchelewa kulipia leseni ya biashara ni asilimia 25 hadi 49 ya ada ya leseni Iwapo mfanyabiashara atakutwa hana leseni ya biashara atapigwa faini ya shilingi laki Moja hadi Laki tatu kwa mujibu wa sheria ya leseni ya biashara

2. USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI

Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa ya mwaka 2015 na marekebisho yake 2019 Nyumba za kulala wageni zote ambazo hazina Tourism License (TALA) zinapaswa kulipiwa ushuru wa nyumba za kulala wageni ambao ni 10% ya mauzo kwa mwezi husika.

3. LESENI ZA VILEO

Kwa mujibu wa Sheria ya Leseni za vileo ‘
THE INTOXICATING LIQUORS ACT 1968’ pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2002. Mfanyabiashara anayeuza vileo anapaswa kuwa na leseni ya vileo. Leseni hii hutolewa kwa wafayabiashara wa vileo ambayo hutolewa kila baada ya miezi sita ambapo kipindi cha kwanza leseni hutolewa kuanzia tarehe 01 mwezi wa 4 hadi tarehe 30 mwezi wa 9 na kipindi cha pili huanza tarehe 01 mwezi wa 10 hadi tarehe 31 mwezi machi.

Kumbuka mfanyabiashara anapaswa kujaza fomu ya maombi ambayo itapitishwa na Afisa Afya, Afisa mipango miji na Mwenyekiti wa kamati ulinzi na usalama kwenye kata kisha Kamati ya Vileo Wilaya.

FAINI YA LESENI YA VILEO

Pamoja na Sheria ya vileo Na. 28 ya 1968. Sheria ya fedha Na. 2 ya 2014, Iwapo mfanyabiashara wa vileo atakutwa hajalipia ada ya leseni ya vileo atatozwa Faini inayoanzia shilingi laki Mbili (Tshs. 200,000) hadi shilingi Milioni moja (Tshs.1,000,000) na hii ni kwa mujibu wa sheria ndogo za halmashauri.

4. KODI YA VYUMBA NA VIZIMBA

Kwa Mujibu wa Kanuni za Mamlaka za Miji za Serikali za Mitaa, 2008 (GN Na 242). Kanuni Na. 111 inaelekeza, mtu hataruhusiwa kutoa bidhaa kwa ajili ya kuuza au kuonyesha bidhaa wa ajili ya kuuza katika soko isipokuwa awe amepewa Kizimba/Kibanda amelipa kodi au ada iliyowekwa.

5. LESENI ZA UVUVI

- **Leseni za Vyombo vya Uvuvi:** Leseni hizi hutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009. Leseni za vyombo vya uvuvi hutolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja, kuanzia tarehe 1 Januari hadi 31 Desemba kila mwaka. Leseni za kukusanya mazao ya uvuvi zinakatwa kati ya tarehe 1 januari hadi 31 machi

- Leseni za Kukusanya Mazao ya Uvuvi: Wafanyabiashara wanaokusanya mazao ya uvuvi wanapaswa kupata leseni husika kwa mujibu wa sheria zilizopo. Leseni hizi pia hutolewa kwa kipindi cha mwaka mmoja, kuanzia tarehe 1 Januari hadi 31 Desemba.

Kuhuisha Leseni Zilizoisha Muda Wake

- Wavuvi na wafanyabiashara wa mazao ya uvuvi wanaweza kuhuisha leseni zao kwa hiyari kati ya tarehe 1 Januari hadi 31 Machi kila mwaka bila adhabu yoyote.

- Baada ya tarehe 31 Machi, mdau yeyote atakayekutwa hajahuisha au kukata leseni atalazimika kulipa faini ya asilimia 50 ya gharama ya leseni husika, pamoja na kulipia leseni yenyewe kabla ya kuendelea na shughuli za uvuvi au biashara ya mazao ya uvuvi.

USHURU WA MAZAO YA UVUVI

- Mfanyabiashara wa mazao ya uvuvi anapaswa kulipia ushuru stahiki ili kupata kibali cha kusafirisha mazao hayo.

ADHABU KWA KUKOSA KULIPA USHURU

- Mfanyabiashara yeyote atakayeshindwa kulipa ushuru wa mazao ya uvuvi kwa mujibu wa sheria atalazimika kulipa faini isiyopungua shilingi 200,000 na isiyozidi shilingi 1,000,000, au kifungo kisichopungua mwaka mmoja na kisichozidi miaka miwili, au adhabu zote kwa pamoja

6. KODI YA HUDUMA (SERVICE LEVY)

Kodi /Ushuru wa huduma ni ushuru unaotozwa kwa kiwango cha asilimia 0.3 kwenye mauzo baada ya kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwa kampuni / biashara zilizosajiliwa VAT.

Kodi hii inatozwa kwa mujibu wa sheria ndogo ya Manispaa ya Ilemela ya mwaka 2022.

Je nani anapaswa kulipa kodi hii?

Ni mfanyabiashara yeyote anaefanya biashara ndani ya manispaa ya Ilemela.

TOZO

Kwa kampuni, wafanyabiashara wakubwa na wa kati: ambao wanatunza kumbukumbu ya mauzo hutozwa ushuru wa huduma kwa asilimia 0.3 ya mauzo yao ya biashara husika kwa mwezi baada ya kuondoa VAT, kundi hili la wafanyabiashara wakubwa na wa kati hupaswa kulipia kodi hii kila mwezi baada ya kufunga hesabu au kila baada ua miezi mitatu (yaani kila robo mwaka).

Kundi la wafanyabiashara wadogo;hulipia ushuru wa huduma mara moja kwa mwaka kulingana na kiwango cha leseni ya biashara. Viwango vya kulipa kodi ya huduma kwa wafanyabiashara wadogo kulingana na leseni zao;

VIWANGO VYA KULIPA KODI YA HUDUMA KWA WAFANYABIASHARA WADOGO KULINGANA NA LESENI ZAO;

SN.	VIWANGO VYA LESENI	KIASI CHA KULIPIA KWA MWAKA
1	1 - 50,000	30,000
2	50,000 – 100,000	50,000
3	100,000 – 200,000	70,000
4	200,000 – 300,000	100,000
5	300,000 – 500,000	130,000

Kumbuka; Mfanyabiashara yoyote atakaekwepa kulipa ushuru wa huduma atatozwa faini ya kuanzia shilingi laki mbili (Tshs. 200,000) hadi Shilingi milioni moja (Tshs. 1,000,000) na hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 8(2) cha sheria ndogo.

FAIDA ZA KULIPA USHURU WA HUDUMA

- Mapato yanayotokana na ushuru wa huduma hutumika kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na shughuli za uendeshaji, asilimia 60 ya makusanyo hutengwa kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo.

7. ADA YA KIBALI CHA UJENZI

Kibali cha Ujenzi (Building Permit) ni nyaraka ya ki-sheria inayotolewa na Mamlaka za Upangaji (Planning Authorities) ambazo ni halmashauri za majiji,manispaa, wilaya (The Local Government Authorities) ili kuruhusu Ujenzi mpya au kufanya marekebisho ya jengo.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 35 (i) cha Sheria ya Mipangomiji Na. 8 ya mwaka 2007, na muongozo wa vibali vya ujenzi vilivyotolewa na OR-TAMISEMI wa 2018, mamlaka ya Upangaji inatakiwa kutoa kibali cha Ujenzi katika kipindi kisichozidi siku 30 kuanzia tarehe mwombaji alipowasilisha maombi yake. Aidha, ndani ya muda huo mamlaka inatakiwa kumjulisha mwombaji kuwa amekubaliwa au amekataliwa ombi lake na kutaja sababu zilizopelekea ombi lake kukataliwa.

NYARAKA MUHIMU ZINAZOTAKIWA KWA AJILI YA KUPATA KIBALI CHA UJENZI.

- Nakala ya Hati / offer ya umiliki wa kiwanja
- Nakala ya Risiti ya malipo ya kodi ya ardhi ya kiwanja ya mwaka wa kuomba kibali
- Ramani za majengo kwa mujibu wa matumizi ya kiwanja yaliyopo kwenye hati zilizosainiwa na mbunifu wa majengo aliyesajiliwa
- Nakala ya risiti ya malipo ya zimamoto

NB: Kwa muombaji wa majengo makubwa/maghorofa anatakiwa kuwasilisha michoro ya chuma

Kumbuka; Mmiliki wa kiwanja aliyelipia malipo ya kibali cha ujenzi wakati wa Umilikishaji (Viwanja vya Urasimishaji) atatakiwa kuleta nyaraka tajwa hapo juu katika ofisi za ujenzi kwa ajili ya kuidhinishiwa ramani zake na kisha kupata kibali cha ujenzi ndani ya muda uliowekwa kisheria